

**MAMLAKA ZA NIDHAMU ZASHAURIWA
KUZINGATIA SHERIA NA KANUNI KATIKA UTOAJI
WA MAAMUZI YAHUSUYO MASUALA YA NIDHAMU
KWA WATUMISHI WA UMMA**

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Mamlaka za nidhamu katika Utumishi wa Umma zimeshauriwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia masuala ya nidhamu kwa watumishi wa Umma ili kuhakikisha kuwa kila mtumishi anapata haki na usawa anaostahili katika Utumishi wa Umma.

Wito huo umetolewa mapema wiki hii na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma Bw. Jovin Kitambi katika Mkutano wa dharura wa Tume uliofanyika katika Ukumbi wa Tume Accacia House Jijini Dar es salaam ili pamoja na mengine kupitia na kuamua rufaa zilizokatwa na watumishi wa Umma na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Bw. Kitambi amesema kuwa baadhi ya Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma zinafanya maamuzi kuhusu masuala ya nidhamu bila kuzingatia Kanuni na Taratibu zinazoongoza masuala ya nidhamu hali ambayo inailazimu Tume kuamua kuanza upya kwa taratibu za mashauri ya nidhamu.

Alisema ukiukwaji wa taratibu sio tu hucheleweshwa haki ya mtumishi bali huingiza Serikali katika gharama ambazo sio za lazima.

Mwenyekiti huyo alibainisha baadhi ya dosari zinazojitokeza katika maamuzi ya masuala ya nidhamu kuwa ni pamoja na Mamlaka za Nidhamu kutounda Kamati za Uchunguzi, kutolewa kwa Hati ya Mashtaka na Mamlaka isiyo halali na pia mtuhumiwa kutopewa fursa na haki ya kujitetea.

Kutokana na hali hiyo Bw. Kitambi ametoa wito kwa Mamlaka zote za Nidhamu kuendesha na kusimamia masulaa ya nidhamu kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007, Kanuni na Taratibu zake za mwaka 2003 pamoja na Miongozo na Nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Serikali ili kuhakikisha kila mtumishi anapata haki anayostahili kwa wakati muafaka.

Pamoja na shughuli ya kuamua rufaa, Mwenyekiti wa Tume, Bw. Kitambi aliongoza pia uteuzi wa Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Wilaya na Mikoa za Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) ambazo husimamia maadili ya Ualimu na pia hutoa maamuzi au mapendekezo kuhusu mashauri ya nidhamu ngazi ya Wilaya na Mkoa. Aidha, uteuzi huo umefanyika kufuatia Kamati zilizokuwepo kumaliza kipindi cha miaka mitatu ya utendaji Kisheria Disemba 31, 2010.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Mwenyekiti, Makamishna wa Tume na Sekretarieti ya Tume ya Utumishi wa Umma. Tume hufanya Mikutano yake kwa mujibu wa Sheria ambapo Mikutano hiyo hufanyika kila robo ya mwaka kwa mwaka.

Ikiwa una maoni /ushauri au maswali tafadhali tuandikie:-

***Katibu,
Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P 9143,
Dar es salaam.***